# MSAMAHA NA UPATANISHO

## KITABU CHA KUJIFUNZIA

Na utusamehe dhambi zetu, kama sisi tunavyowasamehe waliotukosea. (Mathayo 6:12)

FDM.WORLD

Craig Caster

*Forgiveness and Reconciliation* in Swahili

FAMILY
DISCIPLESHIP
MINISTRIES

Simu: (619) 590-1901
Barua pepe: info@FDM.world
Wavuti: www.FDM.world

**Msamaha na Upatanisho V. 2.0 na Mchungaji Craig Caster**

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki hakiwezi kubadilishwa au kuhaririwa kwa njia yoyote, au kutolewa tena kama kitabu kamili au sehemu kwa faida binafsi. Kitabu hiki kinaweza kuzalishwa bila gharama; kwa kitabu chote au sehemu kwa kusudi la matumizi ya binafsi au kuwahudumia wengine.

Haki zote zimehifadhiwa.

Isipokuwa imeonyeshwa vingine, marejeleo yote ya Biblia yamechukuliwa kutoka Swahili Union Version, mwaka 1967; Chama cha Biblia cha Tanzania na Chama cha Biblia cha Kenya.

Nakala za ziada zinaweza kupatikana kwa kuwasiliana na:

Huduma ya Uanafunzi katika
Familia 131 Benney Lane, STE B #
102 Dripping Springs, TX 78620
Simu:
(619) 590-1901 Barua pepe:
Team@FDM.world www.fdm.world

## Kuhusu Mwandishi

Mchungaji Craig Caster ndiye Mwanzilishi na Mkurugenzi wa Huduma ya Uanafunzi katika Familia. Mwanzoni mwa 1992 Craig alianza kuhisi msukumo kuhusu familia kutoka kwa Bwana. Wakati huu katika maisha yake Craig alikuwa Makamu wa Rais wa kampuni kubwa inayoendelea huko San Diego, California na alikuwa ametumia miaka 8 kama Muhudumu mzuri akiongoza huduma ya ndoa na vile vile ya vijana. Katika mwaka huo Bwana alianza kufunua maono ya huduma hii na mnamo Januari 1993, Craig aliacha kazi yake kwa ajili ya huduma ya wakati wote. Mnamo 1994 Huduma ya Uanafunzi katika Familia ikawa huduma isiyo ya kibiashara huko San Diego, California.

Craig amepata sifa kati ya makanisa mengi ya kiinjili kama chanzo cha kuaminika katika ushauri wa familia, semina, na rasilimali za huduma ya familia. Ameandaa nyenzo za ndoa na malezi ya kibiblia na amefundisha maelfu kupitia semina zinazohudhuriwa katika makanisa kote nchini na nje ya nchi. Semina hizi za kibiblia zimekumbatiwa na kaunti ya San Diego na inakidhi mahitaji ya wazazi chini ya amri ya korti kuhudhuria masomo ya malezi. Craig amehudumia shule kadhaa na mashirika ya kijamii. Mnamo 1997 Craig aliulizwa na Ofisi ya Wakili wa Jiji la San Diego kusaidia kubuni *Mradi* wao wa *malezi*,na mpango wa kuingilia mapema katika masuala ya vijana wenye matatizo, pia kutoa msaada, na rasilimali kwa wazazi, kwa kushirikiana na idara ya polisi, mashirika ya haki za watoto, na mahakama za nchi .

Kwa kuongezea, chini ya uongozi wa Craig, Huduma ya Uanafunzi katika Familia zilianzisha na kutekeleza huduma ya ushauri kwa watoto wanaotoka familia za mzazi mmoja, vituo vya malezi, na vikundi vya nyumbani vyenya wahudhuliaji zaidi ya 400 kati ya mwaka 1994 na 2000. Kwa zaidi ya miaka 20 iliyopita, Craig amefanya kazi na watoto pamoja na wazazi kama mchungaji mchanga, mshauri wa ndoa, mwalimu, na msahuri.

Craig ameoa tangu mwaka 1980. Yeye na mkewe ni wazazi wa watoto watatu, ambao ni watu wazima sasa pamoja na mjukuu mmoja.

## Kuhusu Huduma ya Uanafunzi katika Familia

Huduma ya Wanafunzi wa Familia ni huduma isiyo ya faida ambayo ilianzishwa mnamo 1994, chini ya Mwanzilishi na Mkurugenzi Mchungaji Craig Caster. Kusudi kuu la huduma hii ni kusaidia, kuelimisha, na kufundisha mwili wa Kristo ili kuhudumia familia kwa ufanisi zaidi. Ili kutimiza lengo hili tunatoa ushauri kuhusu familia, semina za kufundisha juu ya ndoa na malezi, uanafunzi wa kiroho, mafunzo ya uongozi wa Kanisa na mafunzo ya ushauri. Huduma ya Uanafunzi katika Familia pia hutoa vifaa anuwai katika muundo wa video na sauti, vitabu vya kujifunzia, nakala ya karatasi, na rasilimali za mkondoni kwa Kiingereza na pia lugha nyingine kadhaa. Maono ya Huduma ya Uanafunzi katika Familia ni kuyafikia makanisa ya Kikristo, kuwawezesha kufundisha sharika zao katika ndoa na malezi. Hadi leo maelfu ya wazazi kote Amerika na nje ya nchi wamekamilisha mafunzo ya ndoa zetu za kibiblia na madarasa ya malezi yaliyowekwa katika makanisa na pia kupitia madarasa yetu ya bure mtandaoni.

**Jedwali la Yaliyomo**

---

**Enzi kuu ya Mungu** **Ukurasa wa 1**

- Mungu anasimamia!

**Majaribu na Dhiki** **Ukurasa wa 4**

- Majaribu na Dhiki ni sehemu ya Maisha ya Kikristo!

**Gharama ya Kutosamehe** **Ukurasa wa 6**

- Msamaha ni bure, hata hivyo, kutosamehe ni gharama kubwa.

**Kwa nini Usamehe?** **Ukurasa wa 7**

- Sababu nne za kibiblia kwanini tunahitaji kusamehe.

**Upatanisho** **Ukurasa wa 9**

- Ikiwa unahitaji kusamehewa.
- Ikiwa unahitaji kusamehe.

**Kudumisha Ahadi yako ya Kusamehe** **Ukurasa wa 13**

- Kushinda utumwa wa uchungu na kutosamehe.

**Hitimisho** **Ukurasa wa 16**

- Kusamehe ni ushindi, lakini ni ngumu kutosamehe.

** *Isipokuwa imeainishwa vinginevyo, marejeo yote ya Maandiko*

*yamechukuliwa kutoka Swahili Union Version 1967.*

**Enzi kuu ya Mungu**

---

Neno **Mwenye Enzi** inamaanisha **-** *Kumiliki nguvu kuu, hekima isiyo na kikomo, na mamlaka kamili.*

> *"Na watu wote wanaokaa duniani wamehesabiwa kuwa si kitu, naye hufanya kama atakavyo, katika jeshi la mbinguni, na katika hao wanaokaa duniani; wala hapana awezaye kuuzuia mkono wake, wala kumwuliza, Unafanya nini wewe?" - Danieli 4:35*

> *"Ee Bwana, umenichunguza na kunijua. Wewe wajua kuketi kwangu na kuondoka kwangu; Umelifahamu wazo langu tokea mbali. Umepepeta kwenda kwangu na kulala kwangu, umeelewa na njia zangu zote. Maana hakuna neno ulimi wangu, usilolijua kabisa Bwana"*
> *-Zaburi 139: 1-4*

Zaburi 139: 1-18 inafundisha kuwa Mungu anamjua kila mmoja wetu kwa undani, kiasi kwamba kila vitendo na mawazo yetu yanajulikana kwake hata kabla hayajajulikana kwetu. Kabla ya kufungua moyo wako kwa Mungu, kwa kumkubali Yesu kama Bwana na Mwokozi, alijua ikiwa utakuja kwake au la na akakupa chaguo hilo kupitia zawadi ya hiari. Mungu hayuko tayari kwamba yeyote aangamie na anachagua kwamba wote wangemfuata. Lakini kupitia utumiaji wa hiari, yeye humpa kila mtu uhuru wa kumkataa.

Wakati Mungu alipoumba Adamu na Hawa, aliwapa kizuizi kimoja, ambacho ni kutokula kwenye mti wa ujuzi wa mema na mabaya. Walipokaidi kwa kumsikiliza Shetani, wanadamu walipata laana ya dhambi. Katika Adamu, Mungu aliwapa wanadamu uhuru wa kuchagua mema, lakini kwa kutotii alichagua uovu; kwa hivyo, sasa ni ukweli kwamba wote wanaochagua kuwa watoto wa Mungu katika Kristo bado wanaishi katika ulimwengu ulioanguka na wanaguswa na uovu unaowazunguka. Ikiwa hii haikuwa kweli na Mungu angewalinda watoto wake kutoka kwenye shida na maovu yote, watu wangechochewa kumgeukia yeye ili kupata maisha rahisi. Kwa hakika, hii ndiyo hoja ambayo ilianzisha mgongano wa kihistoria mbinguni kati ya Mungu na Shetani juu ya maisha ya Ayubu.

Ndipo Shetani akamjibu Bwana:

> "Ndipo Shetani akamjibu BWANA, na kusema, Je! Huyo Ayubu yuamcha BWANA bure? Wewe hukumzingira kwa ukigo pande zote, pamoja na nyumba yake, na vitu vyote alivyo navyo? Kazi za mikono yake umezibarikia, nayo mali yake imeongezeka katika nchi. Lakini nyosha mkono wako sasa, uyaguse hayo yote aliyo nayo, naye atakukufuru mbele za uso wako." - Ayubu 1: 9-11.

Mungu *alimruhusu* Shetani kuleta uovu juu ya Ayubu kupitia kupoteza mali zake, watoto wake, na mwishowe afya yake. Mungu ni Baba mwenye upendo na *haleti* uovu maishani mwetu; lakini, kwa kusudi lake na kwa faida yetu ya baadaye, yeye *anaruhusu* sisi kuguswa na uovu. Matokeo ya mateso ya Ayubu yalikuwa imani kubwa na urafiki na Mungu.

Ayubu hakuelewa sababu ambayo ilifanya Mungu am*ruhusu* ateseke (Mungu amlitangaza Ayubu kuwa alikuwa mtu mwenye haki katika Ayubu 2: 3), kwa hivyo Ayubu alikuwa na swali la, “*kwanini?*" Kwa sura kadhaa Ayubu anaumia juu ya swali hili, akitafuta jibu la kuridhisha. Mungu hajibu kamwe moja kwa moja lakini anageuza umakini wa Ayubu kwa nguvu na utukufu wake, ambao unaonyeshwa katika uumbaji. Ayubu aliridhika kupitia ufahamu wa kina juu ya ukuu wa Mungu. Tunapoteseka, kama Ayubu, tunatafuta maelezo. *"Kwanini, kwanini, kwanini?"* Moja ya masomo mengi tunayojifunza kutoka kwa Ayubu ni kwamba *"Kwanini?"* ni swali lisilofaa. Badala yake tunapaswa kumwuliza Mungu, *"Je ni nini?"*

◆ **ni nini unachojaribu kunifundisha?**

◆ **Mapenzi yako ni yapi kwangu katika msimu huu wa mateso?**

> *"…Mtu ajaribiwapo, asiseme, Ninajaribiwa na Mungu; maana Mungu hawezi kujaribiwa na maovu, wala yeye mwenyewe hamjaribu mtu. Lakini kila mmoja hujaribiwa na tamaa yake mwenyewe huku akivutwa na kudanganywa. " -Yakobo 1: 13, 14*

*"Ndipo Ayubu akamjibu BWANA, na kusema.*

*Najua ya kuwa waweza kufanya mambo yote,*
*Na ya kuwa makusudi yako hayawezi kuzuilika.*
*Ni nani huyu afichaye mashauri bila maarifa?*
*Kwa maana, nimesema maneno nisiyoyafahamu,*
*Mambo ya ajabu ya kunishinda mimi, nisiyoyajua.*
*Sikiliza, nakusihi, nami nitanena;*
*Nitakuuliza neno, nawe niambie.*
*Nilikuwa nimesikia habari zako, kwa kusikia kwa masikio;*
*Bali sasa jicho langu linakuona.*
*6Kwa sababu hiyo najichukia nafsi yangu, na kutubu*
*Katika mavumbi na majivu. "-Ayubu 42: 1-6*

◆ **Ikiwa hii ni kweli, ni sehemu gani ya maisha yako iliyo nje ya nguvu ya Mungu, hekima, au mamlaka yake?**

________________________________________________________

______________________________________________________________

◆ **Ni siku ipi au hali gani imekugusa ambayo Mungu hakuijua kabla?**

___________________________________________________

> *"Na ndani yake sisi nasi tulifanywa urithi, huku tukichaguliwa tangu awali sawasawa na kusudi lake yeye ambaye hufanya mambo yote kwa shauri la mapenzi yake." -Waefeso 1:11*

◆ **Je! Unapaswa kuitikiaje katika kukatishwa tamaa kwa maisha, shida, mateso, na majaribu?**

Ikiwa Mungu alijua yote yatakayotutokea kabla hatujazaliwa, basi kinachotakiwa ni kwamba kwa kujua kwake mapema tuliamriwa mapema kupitia neema yake kuishi maisha tuliyopewa. Mungu hauzuii uovu kutugusa, au kutuokoa kutoka kwenye uchaguzi wetu mbaya, lakini anaahidi kuwafanyia yote mema katika maisha ya wale waliojitolea kwake (Warumi 8: 28-29).

> *"Nasi twajua ya kuwa katika mambo yote Mungu hufanya kazi pamoja na wale wampendao katika kuwapatia mema, yaani, wale walioitwa kwa kusudi lake. Maana wale aliowajua tangu asili, aliwachagua tangu asili wafananishwe na mfano wa Mwana wake, ili yeye awe mzaliwa wa kwanza miongoni mwa ndugu wengi."- Warumi 8:28- 29*

Kwa mfano, tunaweza kuchagua kuwa na uchungu kwa wazazi ambao walitukatisha tamaa, mwenzi ambaye alituacha, marafiki ambao walitukosea, dereva wa kilevi aliyemuua mpendwa, au tunaweza kuweka imani yetu kwa Mungu aliye mkuu.

Tunapokuja kwa Kristo, tunamwamini Mungu na hatima yetu ya milele. Lazima pia tumwamini yeye na hali zetu za zamani na za sasa; Kristo peke yake ndiye anayeweza kutufariji na kututia nguvu ndani na kupitia majaribu yetu na anaweza kuleta mema kutokana kwa mabaya. Ni kwa kupitia imani yetu na utii kwamba Mungu anaweza na atatupa amani, na kuleta sifa, heshima na utukufu kwa Bwana wetu Yesu Kristo.

Soma mstari ufuatao na andika kwa maneno yako mwenyewe kile inachosemwa katika mstari huu na jinsi unavyoweza kukitumika kwa hali yako ya binafsi.

> *"Ahimidiwe Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, ambaye kwa rehema zake nyingi alituzaa mara ya pili ili tupate tumaini lenye uzima kwa kufufuka kwake Yesu Kristo katika wafu; tupate na urithi usioharibika, usio na uchafu, usionyauka, uliotunzwa mbinguni kwa ajili yenu. Nanyi mnalindwa na nguvu za Mungu kwa njia ya imani hata mpate wokovu ulio tayari kufunuliwa wakati wa mwisho. Mnafurahi sana wakati huo, ijapokuwa sasa kwa kitambo kidogo, ikiwa ni lazima, mmehuzunishwa kwa majaribu ya namna mbalimbali; ili kwamba kujaribiwa kwa imani yenu, ambayo ina thamani kuu kuliko dhahabu ipoteayo, ijapokuwa hiyo hujaribiwa kwa moto, kuonekane kuwa kwenye sifa na utukufu na heshima, katika kufunuliwa kwake Yesu Kristo. ” -1 Petro 1: 3-7*

____________________________________________________________________________
______________

____________________________________________________________________________
______________

____________________________________________________________________________

______________

____________________________________________________________________________

______________

***Majaribu na Dhiki***

---

W **NENO LA MUNGU LINAFUNDISHA KUWA MAJARIBU NA DHIKI NI SEHEMU YA MAISHA YA KIKRISTO.**

> *"Hayo nimewaambieni mpate kuwa na amani ndani yangu. Ulimwenguni mnayo dhiki; lakini jipeni moyo; mimi nimeushinda ulimwengu. ” -Yohana 16:33*

Yesu anatuambia kwamba tunaweza kuwa na amani na kwamba ameushinda ulimwengu, lakini bado katikati ya majaribu tunauliza, "Kwa nini? Kusudi *la Mungu* ni nini? ” Kama vile anayesafisha anaweka dhahabu ghafi ndani ya kisulubisho na kuweka joto ili kutoa uchafu juu ya uso, Mungu huruhusu watoto wake wapenzi

kwenda kwenye kifungu cha mateso ili *kusafishwa* na *kubadilishwa* kuwa kwa sura ya Mkombozi wetu, Yesu Kristo.

> *"Naye ataketi kama asafishaye fedha na kuitakasa, naye atawatakasa wana wa Lawi, atawasafisha kama dhahabu na fedha; nao watamtolea BWANA dhabihu katika haki. " -Malaki 3:3*

Ikiwa tunajiamini kwa wema na kusudi la Mungu, mioyo yetu itajaa upendo, tumaini, na ujasiri wa Yesu Kristo. Wengine wataona haki ya Yesu Kristo ikifanya kazi ndani yetu.

Kumbuka Warumi 8: 28-29

> *"Nasi twajua ya kuwa katika mambo yote Mungu hufanya kazi pamoja na wale wampendao katika kuwapatia mema, yaani, wale walioitwa kwa kusudi lake. Maana wale aliowajua tangu asili, aliwachagua tangu asili wafananishwe na mfano wa Mwana wake, ili yeye awe mzaliwa wa kwanza miongoni mwa ndugu wengi."- Warumi 8:28- 29*

Mungu hasemi *baadhi* ya vitu hufanya kazi pamoja kwa ajili ya mema, bali *kila* kitu. Muhimu ni imani; ikiwa tutachagua kuamini ahadi za Mungu na kumtumaini katika majaribu na dhiki zetu zote, tutashinda na Mungu atatukuzwa. Katika kifungu hiki, *"… kwa wale wampendao Mungu"* , ni wale ambao wamepokea Yesu kama Bwana na Mwokozi, ambayo inajumuisha ufahamu kwamba kusudi la Mungu katika maisha haya ni kutukomboa kutoka kwa nguvu ya dhambi, ambayo hutafsiri kuwa mtu ambaye ana uwezo wa kuchagua haki badala ya uovu, na kisha utukufu kwa Mungu.

> *"Ila Mungu ashukuriwe, anayetushangiliza daima katika Kristo, na kuidhihirisha harufu ya kumjua yeye kila mahali kwa kazi yetu." -2 Wakorintho 2:14*

◆ **Je, uko tayari kumwamini Mungu kwa maumivu ambayo wengine wamesababisha katika maisha yako? Ndio ☐ Hapana ☐**

◆ **Je, uko tayari kuruhusu Mungu kubadilisha maisha yako kwa njia ya majaribio?**

◆ **Je, uko tayari kuamini Mungu ikiwa wewe unakabiliana na machungu na majaribio katika maisha yako?**

> *"Kuna nyakati, anasema Yesu, wakati Mungu hawezi kuondoa giza kutoka kwako, lakini umtumaini yeye. Mungu ataonekana kama rafiki asiye na fadhili, lakini sivyo; atatokea kama Baba asiye wa asili, lakini sivyo; atatokea kama hakimu dhalimu, lakini sivyo. Weka wazo na akili yako nyuma ya Mungu kuhusu vitu vyote, na utakuwa na nguvu na kuendelea. Hakuna kinachotokea haswa isipokuwa mapenzi ya Mungu yapo nyuma yake, kwa hivyo unaweza kupumzika kwa ujasiri kamili kwake. "*
>
> Uwezo wangu kwa alie juu zaidi Oswald Chambers

**Gharama ya Kutosamehe**

Neno *kusamehe* kihalisi linamaanisha *kutoa*. Wakati deni linaposamehewa, haki za malipo *hutolewa*. Kama mtu akiniumiza na nikamsamehe, *nagawa* uhuru wa kuendelea kuwa na hasira na kinyongo kumuelekea yule alienikosea. Kufanya hivyo huvunja ngome nyingi ambazo husababisha shida za—kihisia na kisaikolojia. Kumtumaini Mungu na kuwasamehe wengine inamaanisha kutoa machungu yetu kwa Mungu, kumruhusu ayaondoe kutoka kwetu. Kwa njia hii, tunatoa haki yoyote ambayo tunaweza kuwa nayo kukasirika au kutafuta malipo. Kupitia Mungu, tunatoa msamaha kwa kosa. Neno *msamaha* limetokana na Kilatini, *perdonare*, maana yake *kutoa bure* . Msamaha wa kweli haustahili, hauna ukomo, na ni bure. Sio *haki* au *stahiki*. Katika maandiko, *kusahau* inamaanisha, *kuachilia kutoka kwenye nguvu ya mtu.*

Tunapokataa kutoa msamaha, tukichagua kudumisha *haki* yetu ya kudai malipo ya makosa ambayo tumefanywa, kuna bei ya kulipa. Kutosamehe, au kutokuwa tayari kuacha kosa wakati tunaamini mtu mwingine ametukosea, husababisha hali mbaya ya kihisia. Kitu ambacho ni cha kawaida ni *chuki*, ambayo inamaanisha *kuhisi tena*. **Chuki hushikilia uchungu wa zamani, ukiuwamini tena na tena**. Hasira ni kama *kutoa gamba kwenye kidonda*, inazua vidonda vyetu kupona.

> *"Mkiangalia sana mtu asiipungukie neema ya Mungu; shina la uchungu lisije likachipuka na kuwasumbua, na watu wengi wakatiwa unajisi kwa hilo." - Waebrania 12:15*

♦ Katika Waebrania 12:15, tunajifunza kuwa uchungu ni kama mzizi mzito unaoshika moyoni mwa mwanadamu, ambao hukua na *kuzaa matunda*; lakini, badala ya kustawisha wengine, matunda haya machungu hututia unajisi sisi na wengine.

♦ Watu wengi hawatambui au hukubali kwa utayari kutunza kutosamehe, hasira au uchungu kwasababu tu wanatambua kuwa ni hisia yenye mantiki baada ya kuumizwa. Wanaona hali yao ikiwa ya haki na hutafuta wengine kusikiliza malalamiko yao, au kuwahurumia. Waefeso 4:31 inafundisha kwamba kutakuwa na ushahidi usiopingika katika maisha ya mtu kwamba mti mchungu wa kinyongo unakua ndani ya mioyo yao.

> *"Uchungu wote na ghadhabu na hasira na kelele na matukano yaondoke kwenu, pamoja na kila namna ya ubaya."*
> *-Waefeso 4:31*

**Chuki** - *Mlipuko wa hasira kali, kisasi au ghadhabu, kutafuta malipo*.

**Hasira** - *Hali ya akili inayojulikana kwa ukali na kukabiliana na changamoto za maisha na kuchanganyikiwa.*

**Kunena *Uovu*** - *Maneno yasiyofaa, matusi dhidi ya mtu, kelele / kashfa, kuumiza sifa ya mtu kwa ripoti mbaya, kusengenya, kutukana na kukashifu.*

**Uovu** - *hisia za chuki ambazo tunalea ndani ya mioyo yetu. Tamaa ya kuona mwingine anateseka na / au kujitenga na mtu huyo, hatutaki kufanya kazi kuelekea upatanisho.*

*Jiulize, "Je! Haya ni ya kawaida katika maisha yangu?"*

*• Kiburi • Kujiona kuwa mwadilifu • Kujionea huruma • Usumbufu wa kihisia • Wasiwasi, mvutano na mafadhaiko • Shida za kiafya • Shida za Kula • Hali mbaya ya kujiamini • Ukosefu wa uaminifu katika mahusiano • Ukosefu wa ukaribu katika ndoa • Shida za kishughuli za Kijinsia • Hukumu & kukosoa wengine • Wasiojali sana na kukasirishwa kwa urahisi • Kukosekana kwa amani na furaha • Ushirika uliovunjika na Yesu • Kuogopa kuongoza kama mume • Kuogopa kufuata kama mke*

## Kwanini Usamehe?

Pamoja na uharibifu wa kihisia na kijamii ambao hutokana na kutosamehe, tuna deni la kusamehe kwa sababu:

### ◆ MUNGU ANAAGIZA

Utii kwa Mungu sio hiari. Kuamua ni lini tutatii na hatutatii amri zake husababisha maisha yasiyokuwa na matunda, yasiyofaa na tasa kiroho.

> *"Bali wapendeni adui zenu, tendeni mema, na kukopesha msitumaini kupata malipo, na thawabu yenu itakuwa nyingi; nanyi mtakuwa wana wa Aliye juu, kwa kuwa yeye ni mwema kwa wasiomshukuru, na waovu. Basi, iweni na huruma, kama Baba yenu alivyo na huruma."- Luka 6: 35-36*

> *"Nanyi, kila msimamapo na kusali, sameheni, mkiwa na neno juu ya mtu; ili na Baba yenu aliye mbinguni awasamehe na ninyi makosa yenu. "*
> *-Marko 11:25*

◆ **KWA KUSAMEHE, TUNABEBA SURA YA YESU**

Kama Wakristo, tumeitwa kubeba jina la Kristo kwa ulimwengu uliopotea. Kwa kweli, neno *Mkristo* inamaanisha *Kristo mdogo.* Kristo alionyesha msamaha, alikuja hapa duniani na akafa ili kuanzisha msamaha kwa wenye hatia; kubeba sura yake lazima tuwe tayari kuwasamehe wengine, kama vile Yeye hutusamehe. Kristo aliagiza kanisa kutangaza msamaha. Lazima usamehe wengine kubeba sura ya Kristo ndani yako!

> *"Yesu akasema, Baba, uwasamehe, kwa kuwa hawajui watendalo. Wakagawa mavazi yake, wakipiga kura." -Luka 23:34*

> *"Yeye asemaye ya kuwa anakaa ndani yake, imempasa kuenenda mwenyewe vile vile kama yeye alivyoenenda." -1 Yohana 2: 6*

◆ **MSAMAHA UNAVUNJA MZUNGUKO WA UCHUNGU, LAWAMA NA VISASI**

Msamaha huleta uponyaji kwa mtu anayeumia, hufanya kazi kama dawa ya sumu ya uchungu; hata hivyo, haishughulikii masuala yote ya lawama na haki, lakini mara nyingi huzidharau hizo kabisa. Kumbuka, maumivu na chuki huachwa nyuma na Mungu, wakati utii kwa msamaha huleta uhuru na humwezesha mtu kuanza upya katika uhusiano, wakati hiyo inatumika.

Ukweli huu umeonyeshwa katika maisha ya Yusufu, Mwanzo sura ya 37-45. Alisalitiwa na ndugu zake na kuuzwa utumwani, alikataa kuruhusu mzizi wa uchungu ushike maishani mwake. Baada ya kutengana kwa miaka, wakati familia ilipounganishwa, Yusufu alishuhudia kazi ya uponyaji ambayo Mungu alikuwa ameifanya katika maisha yake kupitia msamaha, iliyoonyeshwa na majina ya wanawe.

Katika Mwanzo 41: 51-52, tunasoma:

> *"Yusufu akamwita jina lake yule aliyezaliwa kwanza, Manase, maana alisema, Mungu amenisahaulisha taabu zangu zote, na nyumba yote ya baba yangu. Na wa pili akamwita jina lake Efraimu, maana alisema, Mungu amenipa uzazi katika nchi ya mateso yangu."*

Katika mstari huu, *kusahau* haimaanishi kukoma kukumbuka, lakini inamaanisha *kuachilia*, au kuacha kuumia na kudhibiti maisha yako ya sasa. Yusufu alipata *mafanikio ya* mara moja kwa moja na kuweka imani yake katika Mungu Mwenyezi na kusamehe wengine. Kumbuka kwamba chuki inamaanisha *kuhisi tena.* Badala ya kuzidisha maumivu yake kwa kuihisi mara kwa mara, Yusufu alichagua kumwamini Mungu kama msimamizi wa matukio yote maishani mwake.

*Kutosamehe hutufunga tubaki zamani na hufunga uwezekano wowote wa maisha yenye matunda.*

Wakati wa miaka ya Yusufu huko Misri, alimruhusu Mungu kuponya moyo uliovunjwa na kaka zake. Baadaye, alipopewa fursa, alionyesha uponyaji wake kupitia vitendo vya upendo, msamaha, na neema kwa ndugu zake. Yusufu anazungumza nao katika Mwanzo 45:5.

> *"Basi sasa, msihuzunike, wala msiudhike nafsi zenu, kwa kuniuza huku; maana Mungu alinipeleka mbele yenu kuhifadhi maisha ya watu. "*

Hakukuwa na lawama na hakuna maelezo yaliyodaiwa, isipokuwa tu sauti ya rehema na msamaha. Njia ilisafishwa kwa yusufu na kaka zake kuungana tena na kuanza uhusiano mpya.

◆ **MSAMAHA HULEGEZA VIFUNGO VYA HATIA KWA MKOSAJI**

> *"Ili katika zamani zinazokuja audhihirishe wingi wa neema yake upitao kiasi kwa wema wake kwetu sisi katika Kristo Yesu.*
> *-Waefeso 2: 7*

Msamaha huleta uhuru kwa wote wanaohusika. Mungu alimwacha Yusufu huru, lakini kaka zake wangebeba huzuni yao hadi kaburini ikiwa Yusufu asingewasamehe. Kumbuka, tunasamehe kwa sababu Mungu hutusamehe katika Kristo. Msamaha uleule usiostahiliwa na ambao haujapatikana, ndio tunachodaiwa kwa wengine na hufanya kazi ili kupunguza mzigo wa kukandamiza wa kile tunachojua kama hatia.

Ikiwa Yesu asingeweza kutoa fadhili na msamaha kwa wenye dhambi, sisi sote tungekuwepo katika vifungo vya hatia milele. Alifanya hatua ya kwanza kuelekea kwetu, ambayo ilifanya iwezekane sisi kupatanishwa naye.

**Upatanisho**

*Kupatanisha* ni kurejesha urafiki au maelewano, hata daraja au kutatua tofauti. Ni kuondoa uadui, kukomesha ugomvi. Upatanisho unamaanisha kuwa pande zilizokuwa zikipatanishwa hapo awali-zilikuwa na uhasama na / au zilitengana.

**KUMBUKA:** kuna hali ambapo maridhiano *si* lazima, inawezekana, au hata inahitajika, katika mazingira kama vile:

- Mzazi anayemnyanyasa kihisia au kimwili au mwenzi wa zamani.
- Mtu wa mwingine tu ambaye alikuumiza wewe au mpendwa wako: mbakaji, mlevi ambaye aliumiza au kumuua mpendwa, mwalimu au mkufunzi aliyekuumiza kwa maneno, n.k.

Hekima inatumika wakati wa kuzingatia upatanisho, ambayo ni tofauti na msamaha. Kwenye mahusiano yetu yote, kuanzisha mipaka kwaajili ya ustawi wa kihisia na kimwili ni muhimu. Na upatanisho wowote unaokwenda kwa mafanikio utaambatana na wema na amani badala ya hasira na misukosuko.

> *"Uchungu wote na ghadhabu na hasira na kelele na matukano yaondoke kwenu, pamoja na kila namna ya ubaya; 32*tena iweni wafadhili ninyi kwa ninyi, wenye huruma, mkasameheane kama na Mungu katika Kristo alivyowasamehe ninyi."*
> *-Waefeso 4: 31- 32*

Maandiko yanatuelekeza *"Uchungu wote… uondolewe mbali na wewe… uwe mwema… mwenye huruma, mwenye kusamehe…"* Hutuongoza na kutuelekeza katika kila moja ya maswali haya.

◆ **Tunaondoaje uchungu?**

◆ **Je! Tunajipatanishaje na mtu ambaye tumemkosea?**

◆ **Je! Tunaponya vipi moyo wa maumivu ambayo tumewasababisha wengine?**

◆ **Tunamsamehe vipi mtu ambaye ametukosea?**

◆ **Tunawezaje kubadili hisia zetu kuhusu makosa yaliyofanyika?**

**Ikiwa Unahitaji Kusamehewa**

***Kama kitendo cha upendo, lazima:***

1. **KIRI DHAMBI YAKO KWA MUNGU, MUOMBE AKUSAMEHE NA KWA ROHO WAKE MTAKATIFU AJAZE MOYO WAKO NA UPENDO WAKE.**

*"Heri aliyesamehewa dhambi na kusitiriwa makossa yake…*

*Niliponyamaza mifupa yangu ilichakaa,*

*Kwa kuugua kwangu mchana kutwa.*
*Kwa maana mchana na usiku*
*Mkono wako ulinilemea.*
*Jasho langu likakauka hata nikawa*
*Kama nchi kavu wakati wa kaskazi.*
*Nalikujulisha dhambi yangu,*
*Wala sikuuficha upotovu wangu.*
*Nalisema, Nitayakiri maasi yangu kwa BWANA,*
*Nawe ukanisamehe upotovu wa dhambi yangu." -Zaburi 32: 1,3-5*

> *"Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote." - 1 Yohana 1: 9*

*"Kama mashariki ilivyo mbali na magharibi,*

*Ndivyo alivyoweka dhambi zetu mbali nasi." -Zaburi 103: 12*

- **Chukua muda sasa kumlilia Mungu, ukimwomba akusamehe na akujaze na Roho wake Mtakatifu ili kukuimarisha wewe kutii.**
- ***Mungu peke yake husamehe dhambi. Yeye husamehe na anasahau. Kwa imani, kubali msamaha kamili wa Mungu na utakaso.***

> *"Msamaha sio hisia … Msamaha ni kitendo cha mapenzi, na mapenzi yanaweza kufanya kazi bila kujali uchungu wa moyo."*
>
> -Corrie ten Boom

2. **IKIWEZEKANA, NENDA KWA WALE WEWE ULIYOWAKOSEA, KWA UNYENYEKEVU UKAUNGAMA NA UOMBE MSAMAHA WAO.**

> *"Basi ukileta sadaka yako madhabahuni, na huku ukikumbuka ya kuwa ndugu yako ana neno juu yako, 24 - iache sadaka yako mbele ya madhabahu, uende zako, upatane kwanza na ndugu yako, kisha urudi uitoe sadaka yako." Mathayo 5: 23-24*

Andika kujitolea kwako kutii Mathayo 5: 23-24.

_________________________________________________________________

__

_________________________________________________________________

__

_________________________________________________________________

__

___________________________________________________________________________

Andika majina na maelezo kwa kifupi kuhusu kile kinachohitajika kusema kwa ajili ya msamaha kutoka kwa kila mtu.

___________________________________________________________________________

___________________________________________________________________________

_________________________________________________

___________________________________________________________________________

___________________________________________________________________________

Maneno sita yenye nguvu zaidi
katika lugha ya Kiingereza:
**"Nilikosea. Tafadhali nisamehe.**

Ikiwezekana, fanya hivi ana kwa ana. lakini, kwa sababu ya usafirishaji au makabiliano yanayowezekana, unaweza kulazimika kuwasiliana na mtu huyo kwa simu au kwa maandishi.

**Kumbuka:** Usiruhusu usumbufu au vizuizi vingine kuchelewesha kitendo hiki cha utii. Katika jamii yetu ya kisasa, simu, huduma ya posta, barua pepe, na meseji inatuwezesha kuwasiliana na wengine haraka.

Shirikisha uamuzi wako kwa rafiki wa Kikristo anayeaminika, umwombe washiriki katika maombi na wewe na uwajibike kukamilisha ahadi hii.

**Kumbuka:** Ikiwa mtu uliyemkosea amekufa, unahitaji kwenda kwa Mungu na ungamo lako.

**TUMIA MUDA WA KILA SIKU NA BWANA KATIKA NENO LAKE NA MAOMBI.**

Moja ya matokeo mabaya mengi ya kutotafuta au kutoa msamaha ni *uhusiano uliozuiliwa na Mungu*.
Tumsifu Bwana kwamba huwa hatuachi kamwe au kututupa, lakini mioyo wetu ndio inakua isio na huruma na kuhisi kujitengwa na hivyo kuathiri uhusiano wetu na yeye. Ninaamini haya ni *matokeo* ambayo Mungu ameunda kutuhamasisha sisi kutoa msamaha katika maisha yetu.

> *"Bali utafuteni kwanza ufalme wake, na haki yake; na hayo yote mtazidishiwa." -Mathayo 6:33*

Andika uamuzi wako wa kutumia wakati na Mungu *kila siku* katika kusoma Neno lake, maombi na kutafakari.

___________________________________________________________________________

_

## 4. TAFAKARI MAANA YA MSALABA NA SADAKA ALIYOFANYA YESU KWA AJILI YA DHAMBI ZAKO.

> *"Maana hapo zamani sisi nasi tulikuwa hatuna akili, tulikuwa waasi, tumedanganywa, huku tukitumikia tamaa na anasa za namna nyingi, tukiishi katika uovu na husuda, tukichukiza na kuchukiana. Lakini wema wake Mwokozi wetu Mungu, na upendo wake kwa wanadamu, ulipofunuliwa, alituokoa; si kwa sababu ya matendo ya haki tuliyoyatenda sisi; bali kwa rehema yake, kwa kuoshwa kwa kuzaliwa kwa pili na kufanywa upya na Roho Mtakatifu." -Tito 3: 3-5*

Chukua muda sasa na umshukuru Yesu kwa yote ambayo amekufanyia: kwa kusamehe dhambi zako zote; kwa mpango wake kamili wa kukugeuza kuwa mfano wake na kwa zawadi ya Roho wake Mtakatifu.

**UKIHITAJI KUSAMEHE**

1. **OMBA NA KUMUOMBA MUNGU NGUVU YA KUTII NA KUSAMEHE MTU AU WATU.**

> *"Yesu akajibu, akawaambia, Amin, nawaambia Mkiwa na imani, msipokuwa na shaka, mtafanya si hilo la mtini tu, lakini hata mkiuambia mlima huu, Ng'oka, ukatupwe baharini, litatendeka." -Mathayo 21:21*

**Mungu aliahidi kutupa nguvu ya kuhamisha milima. Hii inaweza kuwa Mt. Everest!**

> *"Wakati wowote ninapojiona mbele za Mungu na kugundua kitu ambacho Bwana wangu aliyebarikiwa amenifanyia pale Kalvari, niko tayari kumsamehe mtu yeyote chochote, siwezi kuizuia. Sitaki hata kuizuia. "*
> *-Dkt. Martyn Lloyd-Jones*

Tunajua kwamba ni mapenzi ya Mungu kwamba tuwasamehe wengine, kwa hivyo tunaweza kuwa na hakika kwamba ikiwa tutaomba nguvu hii, tutapewa.

2. **WASILISHA NA MSAMAHA WAKO KWA MTU AU WATU.**

> *"Na huu ndio ujasiri tulio nao kwake, ya kuwa, tukiomba kitu sawasawa na mapenzi yake, atusikia." -1 Yohana 5:14*

> *"Basi kama ni hivyo, na mfuate mambo ya amani na mambo yafaayo kwa kujengana." - Warumi 14:19*

**Hamasishwa!**

Katika Mathayo 22: 36-40, Bwana Yesu alifunua ukweli muhimu wakati akijibu swali hili: *"Mwalimu, ni ipi amri kuu katika sheria?" Yesu akamwambia, "Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote na kwa akili zako zote."*

*Hii ndiyo amri ya kwanza na kuu. Na ya pili ni kama hiyo: 'Mpende jirani yako kama nafsi yako.' Juu ya amri hizi mbili hutegemea Sheria yote na Manabii. ”* Yesu mwenyewe alisema kuwa upendo wetu kwa wengine ni muhimu sawa na upendo wetu kwake.

Tunataka Mungu atusamehe na, kwa kweli, tunaomba hii mara kwa mara na tunategemea. Mungu anaonyesha upendo wake kwetu na tunapaswa kujibu kwa kumpenda kwanza na kisha kuwapenda wengine. Mstari huu HAUSEMI kwamba upendo wetu kwa wengine utatuweka katika mgogoro na matakwa ya Mungu au mapenzi yake kwetu, lakini kwamba upendo wote ambao tunaonyesha kwa wengine utakuwa ndani ya wigo wa utii wetu kwake. Hatutaweka tamaa zetu wenyewe au shauku ya kuridhisha wengine juu ya utii wetu kwa Mungu.

Mathayo 5:22 inasoma, *“Bali mimi nawaambieni, Kila amwoneaye ndugu yake hasira itampasa hukumu; na mtu akimfyolea ndugu yake, itampasa baraza; na mtu akimwapiza, itampasa jehanum ya moto.”*

Tufafanue kwa uwazi maneno katika mstari huu. Kuwa na "hasira juu ya ndugu yake" inamaanisha; kumtendea mtu kwa mawazo, maneno au tendo kwa njia isiyo na upendo. Je! Ni kawaida kiasi gani kati ya waumini leo kumtendea mwenzi, mtoto, rafiki, mfanyakazi, au hata mgeni, kwa njia isiyo na upendo na kutoa visingizio kwa tabia zao badala ya kutafuta upatanisho?

Neno *kumwapiza* linamaanisha kumweka mtu kwenye fedhea, kuhukumu, au kuamini kuwa hawana maana au wako chini kuliko wewe kwa njia fulani. Neno *mpumbavu* linamaanisha mtu ambaye hana maadili na hastahili wokovu. Haya ni mashtaka mazito ambayo waumini wengi wanawalenga wengine kwa sababu moja au nyingine. Bwana anasema katika 1 Wakorintho 6:20, *“kwa maana mlinunuliwa kwa gharama; kwa hivyo mtukuze Mungu katika mwili wako na kwa roho yako, ambayo ni ya Mungu”.*

Tunapaswa kumtukuza au, kwa maneno mengine, kumwonyesha Kristo kwa wote bila ubaguzi. Mawazo au tabia zinazoendelea kwa wengine ambazo hazipendi au sio za Kristo hazina sababu na zinahitaji ***toba*** kwa Mungu na kwa mtu huyo. Mathayo 5: 23-24 inasema, *“Kwa hiyo ukileta sadaka yako madhabahuni, na ukakumbuka ya kuwa ndugu yako ana neno juu yako, acha sadaka yako mbele ya madhabahu, uende zako. Kwanza upatane na ndugu yako, halafu njoo utoe sadaka yako”.*

Tunakwenda madhabahuni wakati gani? Hii inamaanisha ushirika wetu na Yesu, wakati wetu katika maombi na shukrani na kumwomba yeye. Ni matendo yetu ya kila siku ya kujitolea na shauku yetu kukaa ndani yake; Yohana 15: 5-6 inasema, *“Mimi ndimi mzabibu, ninyi ni matawi. Yeye akaaye ndani yangu, nami ndani yake, huyo huzaa sana; kwa maana bila mimi hamwezi kufanya neno lo lote”.* Kukaa maana yake ni kukaa na; kuishi katika ufahamu wa mara kwa mara wa kuwa hekalu la Roho Mtakatifu. Na inasema kwamba ***TUKIFANYA*** hivyo, tutazaa matunda mengi, kwani bila *neema* yake hatuwezi neno **lolote**. Kwa hivyo, kwenda madhabahuni inamaanisha ushirika wetu na Yesu na uwezo wetu wa kupokea neema inayohitajika kwa kuzaa matunda na kutii mapenzi yake.

Wakati tunadaiwa msamaha na mtu, iwe kwa kuomba au kutoa, Mungu anasema lazima kwanza tuondoe hii kabla ya kutarajia baraka na neema yake. Sadaka gani katika Mathayo 5:23? *"Basi ukileta sadaka yako madhabahuni…".*

Tunajua kwamba kuleta dhabihu hekaluni ilikuwa kawaida kwa Wayahudi kama sehemu ya upatanisho wa dhambi zao. Sadaka zetu leo ni sifa, zaka, ibada, utii, na huduma kwake. Lakini Yesu alisema hatapokea sadaka hizi ikiwa unadaiwa upatanisho wa mtu yeyote.

I Samweli 15:22 inasema, *"Je! Bwana anafurahiya sadaka za kuteketezwa na dhabihu, kama vile kutii sauti ya Bwana? Tazama kutii ni bora kuliko dhabihu, na kusikiliza kuliko mafuta ya kondoo waume.* Kwa hivyo tunaona kuwa huduma na kufanya kazi kwa Mungu hakutatatua shida hii.

Katika 1 Wakorintho 11: 26-32, tunahimizwa *kujichunguza* wenyewe kabla ya kula ushirika: *"Kwa maana kila mnapokula mkate huu na kunywa kikombe hiki, mnatangaza kifo cha Bwana hata atakapokuja. Kwa hiyo mtu yeyote anayekula mkate huu au kunywea kikombe cha Bwana kwa njia isiyostahili atakuwa na hatia ya mwili na damu ya Bwana. Lakini mtu na ajichunguze mwenyewe, na hivyo ale mkate na anywe kikombe. Kwa maana yeye anayekula na kunywa kwa njia isiyostahili hula na kunywa hukumu yake mwenyewe.* ***Kwa sababu hii wengi wako dhaifu na wagonjwa kati yenu, na wengi wamelala. Kwa maana ikiwa tungejihukumu wenyewe, hatungehukumiwa. Lakini tunapohukumiwa, tunaadhibiwa na Bwana, ili tusipate kuhukumiwa na ulimwengu.*** *"*

Ni mara ngapi Wakristo huja kanisani na kula karamu bila kwanza kuchunguza mioyo yao ili kuona ikiwa wana uchungu na / au wamemkosea mtu, na hawatubu au kupanga kupatanishwa na mtu huyo?

Neno kupatanisha linamaanisha kurekebisha mambo; kubadili hisia au mtazamo kuelekea mwingine; au kulipa deni linalodaiwa.

Warumi 13: 8 inatuambia, *"Msiwe na deni ya mtu yeyote isipokuwa kupendana, kwa maana yeye ampendaye mwenzake ametimiza sheria."* Kama Wakristo tuna deni la kulipa ambalo Mungu mwenyewe anasema tunadaiwa na wengine: kuwapenda kwa mawazo, maneno, na matendo. Hii pia ni pamoja na kuwasamehe wale ambao wametuumiza; Wakristo wengi wana uchungu, chuki, au kutosameheana. Wanathibitisha kuhifadhi hisia hizi kwa sababu mtu huyu bado hajalipa matokeo yoyote stahiki na hawavika jukumu lolote kwa tabia yao. Ni ukweli wa maisha kwa watu wote: tutaumizwa na wengine, hata wale ambao wanapaswa kutupenda. Wazazi wetu, ndugu zetu, wenzi wa ndoa, wajomba, shangazi, marafiki, wachungaji, walimu, nk wanaweza kutuumiza kutokana na ujinga na / au kwa makusudi.

Neno *kusamehe* ni kitendo*, au* neno la ***kutenda.*** Mungu anatumia Neno lake kuzungumza nawe hivi sasa, akifunua ukweli wa kuchukua hatua.

Msamaha sio jambo rahisi kufanya, kwa hivyo haupaswi kujaribu kusimama peke yako, lakini tafuta *msaada* na uwajibikaji wa rafiki Mkristo aliyekomaa, mwenzi, au mshirika wa maombi kukusaidia kufuata.

Andika kujitolea kwako kumsamehe mtu huyo, au kuomba msamaha wa mtu ambaye Mungu amekufunulia. Jipe tarehe ya mwisho ya kuwasiliana ili usiisahau!

_________________________________________________________________________

_________________________________________________________________________

_________________________________________________________________________

> *"Kwa maana mkiwasamehe watu makosa yao, na Baba yenu wa mbinguni atawasamehe ninyi."* -Mathayo 6:14

Katika visa vingine, kwa sababu ya usafirishaji, gharama ya kusafiri, usalama kwako, au uwezo wa mtu mwingine kukubali kile unachohitaji kusema; barua, barua pepe, maandishi au simu inaweza kuwa njia bora kwako kutimiza haya.

**<u>Weka hoja hizi akilini wakati unazungumza au unawasiliana kwa maandishi:</u>**

1. **Unafanya hivyo kwa utii kwa Baba yako wa Mbinguni ambaye anakupenda na kukujali.** Anataka uwe huru kutoka kwenye utumwa na uonevu ambao umekuwa ukipata kama matokeo ya kutosamehe.

2. **Sio lazima ujifunze kila undani wa kosa lao dhidi yako.** Mara nyingi, haswa wakati wa kuwasamehe wazazi, hawajui kabisa nini wanaweza kufanya kukuumiza. Katika visa vingine, makosa yanaweza kuwa dhahiri kama vile unyanyasaji wa kingono, mwili, au kihisia, ubakaji, kutelekezwa na mzazi, rafiki, au mwenzi wako, kashfa zilizosemwa dhidi yako, n.k. Basi unaweza kuwa wazi zaidi kwa nini unahitaji kusamehe.

3. **Usijaribu kulazimisha wengine wakubali makosa yao.** Mungu amekuita kutii, sio kuwa wakili wa mashtaka, hakimu, jaji, au kujaribu kuwafanya wakiri kwamba kile walichofanya kilikuwa kibaya!

4. **Iweka kwa ufupi.** Mara nyingi, kwa sababu ya kiwango cha juu cha mihemko, tunaweza kujikuta tukisema vitu ambavyo hatukukusudia na kudhoofisha kusudi la mkutano, barua, au mazungumzo.

5. **Mwishowe (ikiwa inafaa), waombe wakusamehe kwa kuwa na chuki kwao.** Kumbuka kwamba walichoweza kufanya kilikuwa kibaya na cha kukera, lakini uchungu na kutosamehe ni *dhambi sawa na hiyo*.

> *"Katika siku ile Mungu atakapozihukumu siri za wanadamu, sawasawa na injili yangu, kwa Kristo Yesu."* -Warumi 2:16

> *"Kwa hiyo, wewe mtu uwaye yote uhukumuye, huna udhuru; kwa maana katika hayo umhukumuyo mwingine wajihukumu mwenyewe kuwa na hatia; kwa maana wewe uhukumuye unafanya yale yale."* Warumi 2:1

*"Kiwango ambacho nina uwezo na nia ya kuwasamehe wengine ni dalili wazi ya ni kwa kiwango gani nimepata msamaha wa Mungu Baba yangu kwangu." -Phillip Keller*

Mtu ambaye umemsamehe anaweza kuendelea kuwa sehemu ya kawaida ya maisha yako; labda mzazi, baba / mama mkwe, mtoto wako, au mwenzi. Wakati hii iko hivyo, unaweza kukutana na vita kati ya Roho na mwili baada ya kuomba msamaha au kuwa umewasamehe.

> *"Lakini <u>tunda la Roho</u> ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole, kiasi; juu ya mambo hayo hakuna sheria. Na hao walio wa Kristo wameusulubisha mwili pamoja na mawazo yaje mabaya na tamaa zake. Ikiwa tunaishi katika Roho, na tuenende pia kwa Roho. Tusijivune bure tukichokozana na kuhusdiana. " -Wagalatia 5: 22-26*

Uzoefu wa msamaha umekubadilisha, lakini sio lazima ubadilike. Mungu amekuwa na ushindi mkubwa katika maisha yako, akikuleta mahali hapa pa kujisalimisha na kutii; lakini, msimamo wao na / au tabia yao ya ukali inaweza kuwa haijabadilika! Na wanaweza kuendelea kushikilia uchungu kwako; hali hii itahitaji umtafute Mungu *kila siku* na pengine kwa wakati huu ili *nguvu yake* iendelee kwenye njia yako ya huruma na wema.

Kwa mfano, unamsamehe mzazi kwa kuwa mkali na asiye na upendo, waulize wakusamehe kwa kuwa na uchungu, lakini wanaendelea kuwa wakali na wasio na upendo. *Mwili* wako unaweza kutaka kuguswa jinsi ulivyofanya zamani, lakini Mungu atakuwa mwaminifu kutoa tunda lake maishani mwako *unapojikabidhi* kwake kila wakati.

> *"Enyi watoto, watiini wazazi wenu katika Bwana, maana hii ndiyo haki."*
> *-Waefeso 6:1*

Lazima *kukumbuka* kwamba utii wako katika msamaha haukuwa ili mtu mwingine au watu wabadilike. Mpaka wakabidhi maisha yao kwa Bwana, wao la *hawawezi* kubadilika. Ni ***Mungu*** tu anayeweza kubadilisha mioyo yetu na kufanya upya akili zetu, lakini itatokea tu tunapojikabidhi kwake.

Tunahusika katika vita vya kiroho kila siku. Adui, Shetani, hataki umtii Mungu au ushinde dhambi na maumivu; kwa hivyo, atashambulia akili yako na kumbukumbu ya zamani, mawazo mabaya, uwongo, majaribu na kulaani. Lazima *u* tumie akili kujidhibiti na kukumbuka *kile* na *ambao* unapigana nao!

> *"Basi uvueni uongo, mkaseme kweli kila mtu na jirani yake; kwa maana tu viungo, kila mmoja kiungo cha wenzake. Mwe na hasira, ila msitende dhambi; jua lisichwe na uchungu wenu bado haujawatoka; wala msimpe Ibilisi nafasi." - Waefeso 4: 26-27*

Huu ndio ukweli ambao tunauishi! Shetani anachukia kupoteza nafasi maishani mwako. Hapendi wazo kwamba amepoteza uwezo wa kukuibia amani na furaha ya Mungu.

- **Je, NAACHAJE KUMPA SHETANI NAFASI ZA KUFANYA UHARIBU KATIKA MAISHA YANGU?**

1. **Jaribu kila wazo linaloingia akilini mwako kwa Neno la Mungu ili uone ikiwa limetoka kwake, kwa mwili wako, au kutoka kwa adui.**

*"Maana ingawa tunaenenda katika mwili, hatufanyi vita kwa jinsi ya mwili; (maana silaha za vita vyetu si za mwili, bali zina uwezo katika Mungu hata kuangusha ngome;) tukiangusha mawazo na kila kitu kilichoinuka, kijiinuacho*

*juu ya elimu ya Mungu; na tukiteka nyara kila fikira ipate kumtii Kristo." -2 Wakorintho 10: 3-5*

*"Hatimaye, ndugu zangu, mambo yo yote yaliyo ya kweli, yo yote yaliyo ya staha, yo yote yaliyo ya haki, yo yote yaliyo safi, yo yote yenye kupendeza, yo yote yenye sifa njema; ukiwapo wema wo wote, ikiwapo sifa nzuri yo yote, yatafakarini hayo." - Wafilipi 4: 8*

2. **Omba katika kila tukio, ukiomba nguvu ya Mungu kufanya mapenzi yake.**

*"Usishindwe na ubaya, bali uushinde ubaya kwa wema." -Warumi 12:21*

*"Basi Mungu wa tumaini na awajaze ninyi furaha yote na amani katika kuamini, mpate kuzidi sana kuwa na tumaini, katika nguvu za Roho Mtakatifu." -Warumi 15:13*

3. **Pinga na Mkatae shetani kwa jina la Yesu - PAMBANA!**

"Lakini Mikaeli, malaika mkuu, aliposhindana na Ibilisi, na kuhojiana naye kwa ajili ya mwili wa Musa, hakuthubutu kumshitaki kwa kumlaumu, bali alisema, Bwana na akukemee!" - Yuda *1: 9*

*"Basi nyenyekeeni chini ya mkono wa Mungu ulio hodari, ili awakweze kwa wakati wake; huku mkimtwika yeye fadhaa zenu zote, kwa maana yeye hujishughulisha sana kwa mambo yenu. Mwe na kiasi na kukesha; kwa kuwa mshitaki wenu Ibilisi, kama simba angurumaye, huzunguka-zunguka, akitafuta mtu ammeze. Nanyi mpingeni huyo, mkiwa thabiti katika imani, mkijua ya kuwa mateso yale yale yanatimizwa kwa ndugu zenu walioko duniani." -1 Petro 5: 6-9*

*"Maana naliandika kwa sababu hii pia, ili nipate bayana kwenu kwamba mmekuwa wenye kutii katika mambo yote. Lakini kama mkimsamehe mtu neno lo lote, nami nimemsamehe; kwa maana mimi nami, ikiwa nimemsamehe mtu neno lo lote, nimemsamehe kwa ajili yenu mbele za Kristo, Shetani asije akapata kutushinda; kwa maana hatukosi kuzijua fikira zake. " -2 Wakorintho 2: 9-11*

Mungu anataka ujue mbinu za shetani ili uweze kupata ushindi. Kutosamehe ni moja wapo ya mbinu kali za Shetani kuwaweka watu wa Mungu katika vifungo! Yesu alituonyesha umuhimu wa kutumia Maandiko kupambana na udanganyifu na uwongo wa maadui (Math 4: 4, 7, 10). Kuwa na *mpango wa utekelezaji* kwa kutumia Maandiko hapo juu, na Maandiko mengi katika somo hili *kupambana* na mawazo yoyote yasiyokuwa ya kibiblia kwa mtazamo wa Mungu. Tumia kadi za faharisi 3x5 kuandika Maandiko juu. Kisha jaribu kukariri kwa kuzibeba mfukoni na kuzipitia asubuhi na usiku. Unapoomba na kukariri Maandiko haya utaficha Neno la Mungu moyoni mwako (Zab 119: 11), na utaweza kunukuu Maandiko, kwako mwenyewe kuimarisha ukweli, kuchukua nafasi ya mawazo mabaya, na kwa adui kama Yesu alifanya hivyo. Wakati adui alipomletea Yesu uwongo, Yesu alisema, "*imeandikwa*" (Math 4: 4, 7) na kumnukuu maandiko, tunapaswa kufanya hivyo pia. Ukweli utashinda daima.

**Unaweza Kuhitaji Kuweka Mipaka**

Ni muhimu kujua kwamba unapotoa au kuomba msamaha, haimuachilii mtu mwingine kukuchukulia bila heshima na / au kwa ukali. *Mfano:* mama yako alikuwa

mkali sana au mwenye nguvu wakati ulikuwa unakua na aliendelea baada ya kuhama, kuolewa, n.k. Baada ya kumsamehe, unaweza *kuweka mipaka* ya uhusiano: "Mama, nataka uhusiano na wewe lakini ninahitaji kuanzisha mipaka. Ninahitaji uzungumze nami kwa njia ya upendo na ninaahidi kufanya vivyo hivyo kwako.

Ikiwa yeyote kati yetu anasema jambo lisilo la fadhili kwa mwenzake, tunaweza kusema 'hiyo inaumiza' na / au 'Natamani kutozungumza juu ya mada hiyo ", basi tunahitaji kuomba msamaha na / au kuacha kuizungumzia.

Ikiwa mipaka hiyo haitaheshimiwa, basi nitaondoka / nitakata simu na hatutazungumza kwa siku chache. Mama, njia pekee ambayo tunaweza kujua ikiwa tunataka kuwa na uhusiano ni kwa njia ya kupendana na kuheshimiana. ”

**◆ Je! Ikiwa mtu ambaye ninahitaji kumsamehe ni marehemu? Je! Bado ninaweza kuwasamehe?**

Uchungu huendelea kuishi moyoni mwa mwanadamu muda mrefu baada ya kitu cha uchungu huo kufa. Ni muhimu sana kuona msamaha kama dawa yenye nguvu ya kuponya roho ya hali nyingi mbaya; pokea hii "dawa" na Mungu anaweza kuleta uponyaji, hata jaza uwazi ambao unasumbua roho yako. Kifo cha mkosaji hakifuti Neno la Mungu; msamaha wa kibiblia unahitaji sisi kuchukua hatua . Lazima uanze na kukiri kwa Bwana: *kukiri* inamaanisha *kubali au kufunua makosa ya mtu, kosa au dhambi.* Inasaidia kufanya ukiri wako kwa sauti na kuelezea msamaha wako kwa mtu aliyekufa mbele ya rafiki, mwenzi, mchungaji, mshauri n.k.

**Tumia sala ifuatayo kukusaidia kukuongoza:**

*“Bwana Yesu, asante kwa kufa msalabani na kunisamehe dhambi zangu zote. Ninakubaliana na Neno lako kwamba lazima nimsamehe mtu huyu kwa maumivu waliyonisababishia. Ninakuomba nguvu ya kutii na kusema maneno haya ya msamaha.*

*Nasamehe… kwa…. Ninakuomba uondoe machungu yangu na unisamehe kwa kushikilia hii kwa muda mrefu. Katika Jina la Yesu naomba. Amina”*

**◆ Je! Ikiwa mtu ambaye ninamsamehe hataki kupatanisha uhusiano?**

Lazima uzingatie kuwa unawajibika tu kwa sehemu yako ya upatanisho. Bila kujali msimamo mtu mwingine anachukua, lazima umtii Mungu kwa kuomba msamaha na kutoa msamaha. Ikiwa mtu huyo mwingine anakataa kukupa msamaha au hawakubali makosa yao kwako, Mungu bado atakubariki kwa utii wako na kutoa amani, neema na rehema zake juu ya maisha yako. Bado utapata uhuru wake kutoka utumwani.

Huwezi kuweka *matarajio* yoyote au *mahitaji* juu ya kile mtu mwingine anaweza kusema au kufanya, lakini toa yote kwa Bwana na *umwamini yeye* afanye kazi katikati ya hali zako. Hii ni vita kubwa ya kibinafsi ambayo watu wengi wanakabiliana nayo na tendo hili la utii.

Hatupaswi kutegemea ufahamu wetu, lakini tutii na kujikabidhi kwa Mungu na mapenzi yake. Ametupa sheria za kiroho kutawala, kulinda na kutuweka huru. Neno lake linatupa ufahamu na maagizo ya jinsi ya kufuata sheria hizi. Mwili wetu, kiburi na woga vitatuzuia tusimwamini na kumtii Mungu katika hali hizi, lakini kwa nguvu ya Roho Mtakatifu, tunaweza kushinda.

*"Mtumaini BWANA kwa moyo wako wote,*

*Wala usizitegemee akili zako mwenyewe;*
*Katika njia zako zote mkiri yeye,*
*Naye atayanyosha mapito yako. " -Methali 3: 5-6*

**Omba sala hii:**

*"Bwana Yesu, ninaomba nguvu ya kukuamini katika mazingira haya. Nisaidie kukumbuka kuwa ninafanya hivi kwa ajili yako. Sitazamii… kwa chochote, bali weka maisha yangu mikononi Mwako. Ninaomba upatanisho na mtu huyu, lakini najua kwamba ninaweza tu kufanya sehemu yangu. Ninaombea… kujisalimisha Kwako ili Utukuzwe. Nakuamini kabisa na matokeo. Katika Jina la Yesu ninaomba. Amina"*

**Hitimisho**

Inaweza kuwa vigumu sana kusamehe, lakini maisha ni ngumu wakati sisi *tunapokuwa* hatusamehe kwa sababu hutuletea dhambi na kukosa kile ambacho Yesu alikifanya kwa ajili yetu juu ya msalaba. Uzoefu wetu wa msamaha wa Mungu unahusiana moja kwa moja na uwezo wetu wa kusamehe wengine. Kuwa tayari kusamehe wengine ni dalili mojawapo kwamba tumetubu dhambi zetu wenyewe, tukatoa maisha yetu, na kupokea msamaha wa Mungu. Moyo uliojitoa kwa Mungu hauwezi kuwa moyo mgumu kuelekea wengine.

*Kiburi na woga hutuepusha na msamaha na upatanisho. Kukataa kujitoa au kuvunjika, kusisitiza haki zako na kujitetea zote ni dalili kwamba kiburi cha ubinafsi kinatawala maisha yako, badala ya Bwana. Wakati hofu ya "vipi-ikiwa...?" inakuteketeza na kukudhibiti, omba imani ya kumwamini na kumtii Mungu. Maadui ni ghali sana kuweka; Mathayo 18: 21-35, inaonya kwamba roho ya kutosamehe itakuweka katika gereza la kihisia.*

> *"Mtu wa kwanza na mara nyingi ndiye anayeponywa kwa kusamehewa ni yule anayesamehe ... Wakati tunasamehe kwa dhati, tunamweka huru mfungwa na kisha kugundua kuwa mfungwa tuliyemuweka huru alikuwa sisi." -Lewis Smedes*